**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO**

SHULE YA SEKONDARI HOROMBO,

S.L.P 186,

**MKUU-ROMBO.**

**Tarehe……………………….**

NAMBA ZA SIMU
MKUU WA SHULE: +255 7843477951 + 255 652190906,
MAKAMU +255 7829211881+255 673546582
E-MAIL: horombosec@rombodc.go.tz
Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi-

________________________________________

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI HOROMBO MWAKA …………………**

## 1.0 UTANGULIZI.

Ninayo furaha kukujulisha kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya Sekondari Horombo iliyopo wilaya ya Rombo Mkoani Kilimanjaro; Tahasusi ya CBG/HKL
Shule ipo kilometa 5 toka kituo cha mabasi Mkuu Wilayani. Ni imani yangu kuwa ufikapo shuleni utatumia vizuri nafasi hii uliyotunukiwa na Taifa lako kusoma kwa bidii na maarifa ili kujiletea maendeleo yako binafsi, kwa familia yako na Taifa kwa ujumla.Hivyo unapokuja shuleni lengo lako liwe ni kujifunza kwa bidii ili kupata elimu bora na endelevu.
Aidha, tunaamini kuwa ili ufanikiwe kimasomo lazima uwe na nidhamu ya hali ya juu. Sheria na kanuni za shule nimekufungashia. Soma kwa makini na ujue kuwa kumcha Mungu ni chanzo cha maarifa.

## 1.1. USAFIRI WA KUFIKA SHULENI

Mwanafunzi akifika Moshi mjini kituo kikuu cha mabasi akitokea popote pale, aulize na kupanda magari yaendayo Rombo kupitia Mwika hadi Mkuu Rombo. Nauli ya kutoka Moshi mjini hadi Mkuu Rombo ni Tshs. 5000/= tu.

Kwa wanafunzi wanaotoka Dar es Salaam au kupitia Dar es Salaam wapande magari ya Dar express, Tilisho, Esther luxury ambayo huja moja kwa moja hadi Rombo.Kwa wanaotoka Dodoma/Singida wapande Shabiby line na Ngasere luxury.Kwa wanaotoka Mwanza na maeneo mengine ya kanda ya ziwa wapande mabasi yanayofika hadi Moshi mjini na kisha kupanda magari yanayoenda Mkuu — Rombo.

Ukifika stendi ya Mkuu - Rombo wilayani chukua usafiri wa pikipiki (bodaboda) gharama ni Tsh 3000/= tu. Mwambie akupeleke Horombo sekondari utafika salama.

Muhula wa masomo utaanza tarehe …………………. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe …………………,mwisho wa kuripoti ni tarehe …………………

## 2. *Mambo Muhimu ya Kuzingatia*

### 2.1 SARE YA SHULE:

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na sare ya shule iliyoshonwa vizuri kwa maadili ya mwanafunzi awapo shuleni. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuja na nguo fupi na zinazobana, atakayekuja nazo hatapokelewa.

i. Sketi mbili (02) rangi ya Orange inayozidi magoti kwa urefu unaokaribia kwenye viatu, mshono — "Rinder box" mbele na nyuma, pembeni marinda madogo matatu.
ii. Mashati mawili (2) meupe {kitambaa cha TETRON T/C 65/35(ALUA)} ya mikono mirefu yasiyobana mwili na yenye vishikizo vya kawaida.
iii. Tai ndefu rangi ya Orange iisiyokuwa na Michirizi
iv. Soksi nyeupe ndefu jozi 2 au zaidi na viatu vyeusi vya kamba visivyokuwa na visigino virefu, jozi mbili.
v. Sweta za shule mbili zenye rangi sawa na sketi (Orange).
vi. Jezi za michezo jozi moja rangi nyeupe
vii. Raba za michezo jozi moja rangi yoyote .
viii. Truck suit rangi ya light blue
ix. Gauni la kushindia (Shamba dress) la rangi ya ugoro draft ndogo (kunguru) mshono wa solo, urefu usiopungua inchi 15 kutoka gotini kwenda chini. Kwa wanafunzi Waislamu washone Hijabu ya rangi ya ugoro kwa ajili ya kushindia. Ushungi na mitandio haviruhusiwi kabisa.
x. Mwanafunzi aje na tochi/ taa ya solar na mwamvuli kwa ajili ya kujikinga na mvua
xi. Kwa wanafunzi Waislamu wanaruhusiwa kuvaa HIJABU nyeupe na sketi ya rangi ya orange.
xii. Mwanafunzi aje na sweta mbili za kuvaa usiku wakati wa masomo ya usiku rangi nyeusi na zisiwe na maandishi wala alama nyingine yoyote.
xiii. Mwanafunzi anapaswa kuwa na T-shirt yenye nembo ya shule kwa ajili ya EK na Clubs and Hobbies, itapatikana shuleni.

**N.B;** Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo nyingine tofauti na sare tajwa.

### 2.2 MAHITAJI YA DARASANI

i. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na vifaa vya darasani kama ifuatavyo:-
ii. Madaftari makubwa(Counter Books Q3/Q4) yasiyopungua nane (8).
iii. Kalamu, rula, penseli, mathematical set,
iv. Scientific calculator(Non programmable),
v. Faili kwa kila somo (kwa masomo ya msingi- principle subjects) kwa ajili ya kutunza mitihani na majaribio.
vi. Madaftari madogo angalau saba(07) kwa ajili ya mazoezi na begi la kubeba madaftari (mikoba hairuhusiwi)
vii. Graph paper kwa wanafunzi wa CBG na Kamusi(Oxford Advanced Learner's Dictionary, 9th edition) kwa wanafunzi wa HKL.
viii. Cheti cha matokeo ya kidato cha nne (Result Slip)

B. **MAHITAJI MENGINE MUHIMU**

i. Ream 1 ya karatasi plain ( isiyo na mistari) A4 kwa mwaka.
ii. Ream 1 Ruled Paper (yenye mistari) kwa mwaka
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika Kwa matumizi yake binafsi.(orodha ya vitabu husika imeambatanishwa) (kiambatanisho na. 5)
iv. Dissecting kit na tray kwa wanafunzi wa CBG. Itakaguliwa wakati akifika shuleni.
v. Scientific calculator (CASIO FX 991) kwa wanafunzi wa CBG tu,kwa atakayetaka kununua duka la shule zinapatikana kwa Tshs 30,000/=
vi. Shuka mbili rangi ya bluu bahari (light blue) iliyokolea, Blanketi moja, mto na foronya
vii. Godoro la futi mbili na nusu
viii. Sanduku la bati 1 (Tranker)
ix. Taulo,kanga/kitenge jozi moja, nguo za ndani za kutosha pamoja na Taulo za kike
x. Sabuni za kufulia na kuogea za kutosha, mafuta ya kujipaka(marashi na mafuta mengine yenye harufu kali na yanayobadilisha rangi ya ngozi hayaruhusiwi)
xi. **Vyombo vya chakula**: Bakuli la cello la plastiki lenye mfuniko la plastiki, kikombe cha plastiki, kijiko na kandambili (Pia vinauzwa duka la shule kwa wale wasiokuja navyo)
xii. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.

**C.VIFAA VYA USAFI**

i. CBG —Squizer 1, jembe 1 yenye mpini na Sabuni ya maji (dex) lita 5
ii. HKL - Hard broom 1, mundu 2 na Sabuni ya maji (dex) lita 5

## 3 .MICHANGO YA SHULE

(a)Michango inayotakiwa kulipwa kwa kila mwanafunzi ni:

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5000 |
| 4. | Nembo | 5000 |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5000 |
| | Jumla | **80,000/=** |

Michango yote ya shule iliyoainishwa hapo juu ilipwe kwenye akaunti Namba;
**40401100033 NMB yenye jina la HOROMBO SEC RECCURENT ACCOUNT**

Mwanafunzi aje na pay slip ya benki siku ya kuripoti.Aidha mchango wa Uendeshaji unaweza kulipwa kwa awamu mbili.

## 4. AFYA

i. Ni **LAZIMA** kila mwanafunzi kuwa na bima ya afya
ii. Wanafunzi wenye bima ya NHIF waje nazo shuleni wakati wa kuripoti.
iii. Wanafunzi wasio na bima watapaswa kulipa shilingi 50400 ili wafanyiwe utaratibu wa kuandikishwa kwenye bima wakiwa hapa shuleni.
iv. Shule haitahusika na gharama za matibabu ya mwanafunzi.

v. Kila mzazi ahakikishe kuwa afya ya mtoto wake imepimwa na daktari wa hospitali au kituo cha afya kabla ya kuripoti shuleni na kila mmoja aje na risiti ya malipo ya vipimo. **Taarifa za vipimo vya afya za zahanati hazitapokelewa.**

## 5.0 **FOMU MBALIMBALI KWA MZAZI NA MWANAFUNZI KUJAZA:**

Fomu mbalimbali za kujazwa na mzazi/mlezi pamoja na mwanafunzi zimeambatanishwa.

5.1 Sheria, kanuni na taratibu za shule zilizoambatanishwa, mwanao azisome vizuri na kuzielewa na awe tayari kufuata maelekezo na taratibu nyingine za shule. Mwisho tunamtakia mwanao safari njema ya kuja hapa Shule ya Sekondari Horombo.

Asante na karibu sana.

SEKONDARI
MKUU·ROMBO

ELINE S.LEMA

MKUU WA SHUL

(KIAMBATANISHO Na. 1

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO**

**SHULE YA SEKONDARI HOROMBO**

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995.

Aidha, shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri mkuu — TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

## Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kikamilifu katika masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kufanya shughuli zote za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule,•
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa kuvaa
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix. Kutunza mali za shule.
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini akiwa shuleni bila idhini ya mzazi/mlezi wake
xii. Mwanafunzi hapaswi kuja na simu wala laini ya simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.
xiii. Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa.
xiv. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
xv. Mwanafunzi hataruhusiwa kurudi nyumbani kipindi chote cha masomo bila kibali maalum toka kwa uongozi wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

(KIAMBATANISHO NO

**Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na.**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo; kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wetu ndani na nje ya shule.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana baina ya mwanafunzi na mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote.
vi. Kusuka nywele .
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na biashara na matumizi ya dawa za kulevya.
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, usagaji, ushoga na ulawiti.
xi. Kwenda kwenye maeneo yasiyoruhusiwa bila kibali maalum.
xii. Kumiliki, kukutwa na laini au kutumia simu ya mkononi isiyoruhusiwa katika mazingira ya shule. Simu zinazotumiwa ni zile zilizoelekezwa na uongozi wa shule tu.
xiii. Kudharau alama za taifa (bendera, wimbo wa taifa nk)
xiv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.
xv. Uharibifu wa mali ya umma na mali za watu wengine kwa makusudi.
xvi. Kukataa adhabu iliyotolewa na mwalimu.
xvii. Kukataa kufanya mazoezi na mitihani

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa. mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. **TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWE**LI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

1. Mkuu wa shule•. **0784347795 [0652190906**
2. Makamu Mkuu wa Shule: **0782921188/0673546582**
3. Mwandamizi Taaluma: 0**765116541/0679116541/0759746302**
4. Mwandamizi Malezi: **0620103296/0693977050**

## MKATABA NA KAULI YA KUKUBALI KUTII SHERA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Mimi ______________________________________________ (Jina la mwanafunzl) Ninakiri kuwa nimesoma na kuzielewa vizuri sheria, kanuni na taratibu za shule kama zilivyoainishwa katika vipengele vyote, na kuwa mara nikiukapo sheria hizo hatua za kinidhamu zichukuliwe kama zilivyoainishwa dhidi yangu.

JINA ..................................................

SAHIHI ..............................................

TAREHE...................................................................

Mimi................................................................... .(Mzazi/MIezi wa

mwanafunz) wa mwanafunzi . . . ... ... .........................(Jina la mwanafunzl)
wa kidato cha.....................tahasusi(comb.) ya............

Nakiri kupokea, kusoma na kuzielewa taratibu zote zilizo kwenye maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari ya Horombo. Iwapo mwanangu atakiuka taratibu hizo nitakuwa tayari kukubali hatua zitakazochukuliwa dhidi yake na shule.

Nitakamilisha mahitaji yote ya shule kwa wakati.

JINA LA MZAZI/MLEZI......................................................................

Namba ya
simu................................................................................

SAHIHI ................................................

TAREHE...................................................

Namba ya simu ya ndugu/Jamaa wa karibu... ...........................................

(KIAMBATANISHO NO 3

PRIME MINISTER'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
HOROMBO SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by a medical Officer in a Government hospital.

STUDENT'S FULL NAME: ………………………………………………………………

AGE:…………………………………………………………………

1. Blood count (Red and White): .…………………………………………
2. Stool Examination: ………………………………………………………
3. Urine Examination:________________________________
4. Eye test:…………………………………………………………………
5. Ear test:…………………………………………
6. Speech test:__________________________________________
7. T.B test:……………………………………………………………………………
8. STD test:

9. Spleen.-……………………………………………………………………………

10. Abdomen:

_______________________________________________________

I l. Additional information from any Physical, Mental, Hereditary diseases ordisabilities:

______________________________________________________________

______________________________________________________________

Treatment after Examination:

______________________________________________________________

MEDICAL CERTIFICATE

I certify that the above-mentioned student has been thoroughly examined by me and found fit/unfit to pursue further education.
SIGNATURE.………………………………………………………………

DESIGNATION/STAMP...………………………………………

DATE:………………………………………………………………

STA TION:…………………………………………………………

## (4) MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

JEDWALI NAMBA 1

| JINA LA KWANZA | JINA LA KATI | JINA LA MWISHO | UMRI | TAREHE YA KUZALIWA |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |

JEDWALI NAMBA 2

ANWANI YA NYUMBANI

| KIJIJI/ MTAA | KATA | TARAFA | WILAYA | MKOA | NAMBA YA SIMU | DINI/DHEHEBU |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | |
| | | | | | | |

JEDWALI NAMBA 3

Majina ya watu 4 watakaohusika kuwasiliana na uongozi wa shuleni endapo utahitaji kuwasiliana

| | JINA | UHUSIANAO | MAHALI ANAPOISHI | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |

BANDIKA PICHA ZA WATU WANAOHUSIKA KUWASILIANA

picha za passport size za hivi karibuni)

karibuni)

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |

NB: Kila mwanafunzi ahakikishe kuwa amebandika picha za watu atakaokuwa anawasiliana nao akiwa shuleni.
Picha hizi zitakaguliwa wakati mwanafunzi atakaporipoti shulen

(KIAMBATANISHO No. 5

VITABU VYA MASOMO

Vitabu vya masomo ya tahasusi husika kwa matumizi binafsi ni kama vifuatavyo lakini vinaweza kubadilika kutokana na mabadiliko ya mtaala ulioboreshwa. Hivyo mwanafunzi awe na tahadhari anaponunua . (Mwanafunzi achague kulingana na tahasusi yake).

1. Chemistry
   i. Raymond chang
   ii. Chand I & Il
   iii. - Rymsden 6th addition
   iv. Advanced chemistry Peter Alctin
   v. Mzumbe book Project-Organin part I - Inorganic part I & Il
   vi. TIE (2024) - Physical Chemistry for Advanced level secondary school students book form five and Six
   vii. TIE (2024) — Organic Chemistry for Advanced level secondary school students book form five and six
   viii. TIE (2024) - General Chemistry for Advanced level secondary school students book form five and six
   ix. TIE (2024) — Inorganic Chemistry for Advanced level secondary school students book form five and six
   x. NGAIZA Physical Chemistry and General Chemistry

2. Biology
   i. Understanding biology
   ii. Biological science
   iii. Function approach
   iv. Biology Chand I & Il
   v. TIE (2024) - Biology for Advanced secondary school students book form five
   vi. - TIE (2024) — Biology for Advanced secondary school students book form six

3. Geography
   i. Principles of physical Geography by Monkhouse J.
   ii. Integrated Approach to Geography by David Waugh
   iii. Msabila D.T ( 2024) Physica Geography for Secondary School. Nyambari Nyangwine Publishers.
   iv. TIE (2024) Practical Geography for Advanced Secondary Schools. TIE.
   v. TIE( 2024) Physical Geography for Advanced Secondary Schoo. TIE.
   vi. Practical Geography for Africa by Pritchard John
   vii. Physical Geography — Bunnet
   viii. Research Methodology by Kothan

4. BAM
   i. TIE. (2023).Basic Applied Mathematics.TIE.

ii. Dass H.K. (2010). Engineering Mathematis. S.Chand and Sons Company Ltd.
iii. J.K.Black House.(2010).Pure Mathematics Book 182.Person Education Ltd.
iv. Shayo L.K.S & Masenge R.W.P . Advance Level Mathematics Vol 2.Dar es salaam Press.

5. VITABU VYA KISWAHILI

RIWAYA

i. KezilahabiE.(2003). Dunia uwanja wa Fujo. Africa Proper Education Network.
ii. Mkufya W.E.. (2007). Ua la Faraja. Mangvore Publishers.
iii. Mungo'ng'o C.G. (2003). Mirathi ya Hatari.Mkuki na Nyota Publishers.
iv. Robert S.(2003).Wasifu wa Siti Binti Saad.Mkuki na Nyota Publishers.

**TAMTHILIYA**

i. Mulokozi M.M (2003).Mukwava wa Wahehe.Africa Proper Education Network.
ii. Mbogo E. (2003).Shujaa Mirambo.Africa Proper Education Network.
iii. Imbuga F. (2004).Usaliti Mjini.East Africa Educarional Publishers Limited.

USHAIRI

i. Nyangwine N.C.M(2003).Fumbo Linaloelea.Mbesa Books Distributors.
ii. Wallah W.B..(2004).Malenga wa Ziwa Kuu.East Africa Educational Publishers Limited.
iii. Ghassani M.K.(2003).Andamo, Msafiri Safarini.Educariona Books Publishers Limited.
iv. Amanzy A.M. (2004).Wosia wa Baba.Abantu Publication Limited.

6. **ENGLISH**

i. Oxford Advanced Learners Dictionary,
ii. Advanced Level English: A Practical Aproach.Nicholaus Asheli,Good Book Publishers.
iii. Literature for advanced level:Godfrey Ruta Bukagile.Nyambari Nyangwine Publishers
iv. English for A level—Oxford.
v. Advanced level English language, structure and stylistic : Nicholaus Asheli
vi. English language paper 2 — Nicholaus Asheli
vii. TIE (2024) — Literature in English for Advanced secondary schools form five
viii. TIE (2024) — Literature in English for Advanced secondary schools form six

## 7. HISTORY

i. Advanced Level History paper one N. A. paper two. Kato Abubakar
ii. Essentials in Advanced History.
iii. Major issues in African History Advanced level - Dar —es —salaam University Press — 1996
iv. TIE (2022) — History for Advanced secondary schools student's book (form five)

v. TIE (2016 ) - History for secondary school form six?